



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**



TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA  
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya LIWALE anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesho vikundi vya wanawake, vijana na watu wenyе ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi **730,306,132.00/=** zimetengwa katika robo ya Tatu (Januari-Machi 2025) ya mwaka wa fedha 2025 kwa Mchanganuo Ufuatao:-

- i. Wanawake Shilingi **292,122,452.8**
- ii. Vijana shilingi **292,122,452.8** na
- iii. Watu Wenyе Ulemavu shilingi **146,061,226.4**

Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- i. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenyе ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri,
  - ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
  - iii. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenyе ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyе ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwengine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
  - iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyе akili timamu na wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa na wanakikundi wenyе umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kuitia mfumo wa kielektroniki (tembelea tovuti: [mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz](http://mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz)) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa kata husika au mtendaji wa kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na afisa mtendaji wa kijiji/mtaa, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo

na taarifa ya akaunti ya benki, leseni ya biashara kwa vikundi vinavyofanya biashara leseni ya udereva na usafirishaji kwa vikundi vinavyoomba vyombo vyaa Usafiri na usafirishaji

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 31 mwezi 03 mwaka 2025

Tangazo hili limetolewa leo tarehe 26.02.2025 na: -

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya LIWALE